

**Jibu:** Miti ya Misunobari tunaisoma katika kitabu cha *Isaya 55:13* na sehemu nyingine baadhi katika biblia.

*Isaya 55:13 "Badala ya michongoma utamea MSUNOBARI, Na badala ya mibigili, mhadasi; Jambo hili litakuwa la kumpatia Bwana jina, Litakuwa ishara ya milele isiyokatiliwa mbali"*

**"Misonubari"** ni jamii moja na miti ya **"Mierezi"**. Tofauti ya Msonubari na mwerezi ni kwamba Misonubari yenyewe haiwi mirefu kama mierezi, na pia ina matawi myembamba kuliko mierezi, lakini kwa sehemu kubwa inafanana kimatumizi na mierezi, ndio maana sehemu karibia zote panapotajwa miti ya Mierezi basi na Misunobari pia inatajwa..

*Zekaria 11:2 "Piga yowe, MSUNOBARI, maana mwerezi umeanguka, Kwa sababu miti iliyo mizuri imeharibika; Pigeni yowe, enyi mialoni ya Bashani, Kwa maana msitu wenye nguvu umeangamia".*

Soma pia **2Wafalme 19:23, Isaya 14:8, Isaya 37:24, Ezeieli 27:5**

**na Ezeieli 31:8.**

**Miti ya Misonubari** na Mierezi ilitumika katika ujenzi wa nyumba za thamani na ilipatikana sana katika nchi ya Lebanoni..

Sasa kwa urefu kuhusu miti ya Mierezi na matumizi yake fungua hapa  
>>>**Mwerezi ni nini?**

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

**Mafundisho mengine:**

**NI LAZIMA KUISHIKILIA IMANI MPAKA MWISHO.**

**Sala ya baraka (Hesabu 6:24-26).**

**Fahamu maana ya Mhubiri 10:9 Mwenye kuchonga mawe  
ataumizwa kwayo;**

**FAHAMU SEHEMU NNE (4) APANDWAPO MWAMINI.**

**MWIMBIE BWANA ZABURI KATIKA NYAKATI ZA FURAHA.**

**Rudi Nyumbani**

Share on:

WhatsApp

Print this post